SIRI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Anwani ya Simu:"MKUUPOLISI"

Numbari ya Simu: (022) 2110734
Unapojibu tafadha li taja:

OFISI YA:
INSPEKTA JENERALI WA POLISI
S L P 9 1 4 1
DAR ES SALAAM
07/08/2015

Kumb: No: **PHQ/SO.I/PS/900/C/VOL.IX/8**

Mkurugenzi Mtendaji,
Radar Security Tanzania Limited,
S. L. P 802,
DAR ES SALAAM.

YAH: MAOMBI YA KUANZISHA KAMPUNI YA ULINZI IITWAYO RADAR SECURITY TANZANIA LIMITED:

Rejea barua yako **RSS/SA/2** ya tarehe **01/08/2015** kuhusu kichwa cha habari hapo juu.

Kibali kimetolewa cha kuanzisha kampuni yako binafsi ya ulinzi ijulikanayo kwa jina la ***Radar Security Tanzania***, katika eneo la Mikocheni Karibu na Mwalimu Nyerere, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es salaam.

Unatakiwa kukamilisha mambo muhimu yafuatayo kabla ya kuanzisha rasmi kampuni yako ya ulinzi:

1. Unatakiwa kuisajili mara moja na kutuletea hapa nakala moja ya usajili wake katika kipindi cha siku 60 kwa kibali mama na siku 30 kwa tawi.

2. Unatakiwa kuhakikisha kwamba askari/walinzi wako utakaowaajiri wawe ni watanzania ambao hawana rekodi zozote za uhalifu.Kwa maana hiyo itakubidi kwanza kabla ya kuajiriwa kwao wachukuliwe alama zao za vidole katika kituo kikubwa cha Polisi katika himaya husika na kutumwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (kitengo cha utambulisho,Makao Makuu ya Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi) ili kuhakikisha kwamba hawana rekodi zozote za uhalifu kwa malipo ya Shs.2000/- kwa kila mtanzania na dola 25 za Marekani kwa kila raia wa kigeni.Ni hivyo hivyo pia kwa wakurugenzi,maofisa na watumishi wengine wa kampuni yako.Rekodi hizo pia nakala zake zitumwe hapa kwa ajili ya kumbukumbu.

SIRI

3. Unatakiwa kuhakikisha kwamba walinzi /askari wako wana sare nzuri yaani kuanzia kofia,shati,mkanda,suruali/sketi,kamba ya filimbi,viatu-buti na soksi za kufanyia kazi ambazo hazifanani kwa njia moja au nyingine na sare za majeshi ya ulinzi na usalama hapa nchini.

4. Askari/walinzi wako wanatakiwa kuwa na filimbi au silaha aina ya Shotgun ambazo zimesajiliwa kihalali na Mamlaka inayohusika kwa utaratibu wa kisheria ambao unatakiwa.

5. Unatakiwa kudumisha na kuandaa utaratibu maalum utakaojulikana na Jeshi la Polisi kuhusu maeneo watakayofanyia kazi walinzi/askari wa kampuni yako kiutendaji. Hii ina maana kwamba mwombaji awe na ofisi ya kuendeshea shughuli za Kampuni yake akitaja Mji, Mtaa na namba ya Nyumba iliko ofisi hiyo.

6. Unatakiwa kuwa na uhusiano wa karibu zaidi na Jeshi la Polisi sehemu yako kiutendaji. Aidha wasilisha nakala ya **"Company Profile"** kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa husika.

7. Walinzi watakaoajiriwa wawe na umri wa miaka kati ya 18 – 45 na siyo wazee.

8. Hakikisha kwamba unawasajili **walinzi wako wote** katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kutuletea nakala za hati zao,vinginevyo kama hutatimiza sharti hilo tutakufutia Kibali cha kuendelea na shughuli binafsi za ulinzi.

9. Unatakiwa pia kuhakikisha kwamba unawalipa vizuri mishahara walinzi/askari wako.

10. Hakikisha silaha zinatunzwa katika ghala lililo imara na salama.

11. Hakikisha walinzi wako wanapata mafunzo ya Polisi Jamii kwa Kushirikiana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa.

12. Kufanya ukaguzi wa askari wanapoingia kazini na wanapokuwa kwenye malindo yao ili kubaini kama wako imara kazini, salama na si walevi.

Inspekta Jenerali wa Polisi anakutakia kila la kheri na mafanikio mema ya kiutendaji kwa nia ya kusaidia azma ya kuzuia uhalifu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mussa .A.Mussa - CP AOD

Kny: INSPEKTA JENERALI WA POLISI

Kny. INSPEKTA JENERALI WA POLISI
TANZANIA

Nakala kwa:- Kamanda wa Polisi,
Mkoa wa Kinondoni,
S L P 9140,
DAR ES SALAAM. - Fuatilia kwa karibu kujua kama anatimiza maelekezo aliyopewa na kama anatoa ushirikiano na Polisi.
- Hakikisha walinzi wake wanapata mafunzo ya Polisi Jamii.

Mkurugenzi Mkuu
Business Registration and Licensing Agency
S . L . P 9393
DAR ES SALAAM - Kama jina hilo litakuwa na utata tuletee ili tuweze kufanya marekebisho.

Mkurugenzi Mtendaji
National Social Security Fund
S L P 1322
DAR ES SALAAM -Hakikisha anatekeleza sharti Na. 8.

Mkurugenzi Mkuu
PPF Pensions Fund
S. L. P. 72473
DAR ES SALAAM - Hakikisha anatekeleza sharti Na.8

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Anwani ya Simu:"MKUUPOLISI"

Nambari ya Simu: (022) 2110734
Unapojibu tafadha li taja:

OFISI YA:
INSPEKTA JENERALI WA POLISI
4 BARABARA YA GHANA,
S. L. P 9141
11483 DAR ES SALAAM

Kumb. Na: PHQ/SO.I/PS/900/C/VOL.XIII/60 **20/02/2019**

Mkurugenzi Mtendaji,
Radar Security Tanzania Limited,
S.L.P 802,
DAR ES SALAAM

YAH: KIBALI CHENYE MASHARTI MAPYA CHA KUENDESHA KAMPUNI BINAFSI YA ULINZI YA RADAR SECURITY TANZANIA LIMITED

Rejea barua yako ya tarehe 19/02/2019 kuhusu kichwa cha habari tajwa hapo juu.

Kibali chenye masharti mapya kimetolewa kwa Kampuni binafsi ya ulinzi ya **Radar Security Tanzania Limited,** Iliyopo Mikocheni wilaya ya Kinondoni mkoani **Dar es Salaam.** Kibali cha awali cha Inspekta Jenerali wa Polisi chenye Kumb. Na: PHQ/SO.I/PS/900/C/VOL.IX/08 cha tarehe 07/08/2015 kimefutwa rasmi kuanzia leo. Aidha kibali hiki kipya hakitaathiri vibali vingine vya matawi vya kampuni hii.

Unatakiwa kukamilisha mambo muhimu yafuatayo katika kuendesha kampuni yako ya ulinzi:-

1. Hakikisha kwamba askari/walinzi utakaowaajiri wawe ni watanzania ambao hawana rekodi zozote za uhalifu.Kwa maana hiyo itakubidi kwanza kabla ya kuajiriwa kwao wachukuliwe alama zao za vidole na kutumwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (kitengo cha utambulisho,Makao Makuu ya upelelezi) ili kuhakikisha kwamba hawana rekodi zozote za uhalifu. Gharama ya huduma hii kwa mtanzania ni TShs.2000/- na dola 25 za Marekani kwa raia wa kigeni. Nakala za Rekodi hizo pia zitumwe hapa kwa ajili ya kumbukumbu.

2. Hakikisha kwamba walinzi /askari wako wanavaa sare ya kitambaa aina ya Takron ya rangi zifuatazo: **Dark blue** (suruali, shati na kofia), **Nyeusi** (suruali, shati na kofia) pamoja na shati rangi **Nyeupe**.

3. Askari/walinzi wako wanatakiwa kuwa na filimbi na silaha ambazo sio za kijeshi. Silaha hizo ziwe zimesajiliwa na Mamlaka inayohusika kwa utaratibu wa kisheria.

4. Endapo kampuni yako itatumia silaha za moto basi hakikisha unatumia silaha aina ya SHORTGUN tu.

5. Andaa na dumisha utaratibu utakaojulikana kwa Jeshi la Polisi kuhusiana na maeneo watakayofanyia kazi walinzi/askari wako. Uwe na uhusiano na mawasiliano ya mara kwa mara na Jeshi la Polisi.

6. Walinzi watakaoajiriwa wawe na umri wa miaka kati ya 18 – 45 na siyo wazee.

7. Walinzi/Askari hao walipwe mishahara stahiki.

8. Hakikisha kwamba unawasajili walinzi wako wote katika mifuko ya hifadhi ya jamii na kutuletea nakala za hati zao,

9. Hakikisha silaha zinatunzwa katika ghala lililo imara na salama lililokaguliwa na kupasishwa na Mkuu wa Polisi wa eneo husika.

10. Walinzi wanapaswa wapate mafunzo ya Polisi Jamii kupitia Kamanda wa Polisi wa Mkoa, wakuu wa polisi wilaya na wengineo.

11. Askari wakaguliwe wanapoingia kazini na wanapokuwa kwenye malindo yao.

12. Uhalali wa kibali hiki utadumu kwa muda wa miaka mitatu (3) kuanzia tarehe ya kutolewa. Baada ya hapo itakupasa uombe kibali kingine cha kuendelea kuendesha shughuli ya ulinzi.

13. Kibali chako kitakoma uhalali wake endapo utakiuka masharti yake.

14. Wamiliki, wakurugenzi, walinzi na watumishi mbalimbali wa kampuni kumbukumbu zao zinapaswa kuingizwa katika kanzi data inayoendelea kuandaliwa.

Jeshi la Polisi linakutakia kazi njema katika kudumisha ulinzi na usalama wa taifa.

.....

N.C. MISSAMA – SACP

Kny: INSPEKTA JENERALI WA POLISI

Kny. INSPEKTA JENERALI WA POLISI
TANZANIA

Nakala kwa:

Kamanda wa Polisi
Mkoa wa Kinondoni,
S.L.P 9140,
DAR ES SALAAM. – kwa taarifa.